



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA



TAREHE: 08/05/2018

**TANGAZO LA MNADA WA KUUZA MAGOGO YA MTI AINA YA MKURUNGU (*Pterocarpus tinctorius*)
YALIYOKAMATWA NA KUTAIFISHWA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI, TANZANIA**

1. Wakala wa Huduma za Misituni Tanzania (TFS), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini unatarajia kuuza kwa mnada wa hadhara magogo ya mti aina ya Mkurungu (*Pterocarpus tinctorius*) ambayo yalivunwa kinyume cha Sheria ya Misituni Na. 14 ya mwaka 2002. Taarifa juu ya mahali, idadi, ujazo wa magogo (m³) na tarehe ya mnada imeonyesha kwenye Jedwali hapa chini.

Kituo	Aina ya magogo	Idadi	Ujazo (m ³)	Tarehe na muda wa mnada		
Momba - Tunduma	Mkurungu	546	128.3	22.05.2018	saa	3.00
Mbozi -Vwawa	Mkurungu	910	128.5	22.05.2018	saa	5.30
Mbeya- Ofisi ya Kanda	Mkurungu	98	10.9	22.05.2018	saa	8.00
Jumla kuu			267.7			

2. Mnada huu utafanyika katika maeneo ambapo magogo hayo yamehifadhiwa kwa muda ulioonyeshwa katika jedwali hapa juu. Mnada huu utafanyika kwa kuzingatia kanuni 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misituni za mwaka 2004. Mnunuzi atatakiwa kujiridhisha na hali ya magogo jinsi yalivyo kabla ya kukubali kununua ili kuepuka malalamiko yanayoweza kujitokeza baada ya mnada kufanyika.
3. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mnada huu lazima awasilishe: (1) Usajili wa kiwanda cha kuchakata magogo au awe na mkataba na kiwanda cha kuchakata magogo kilichosajiliwa (2017/18), (2) usajili wa kufanya biashara ya mazao ya misitu, (3) cheti cha utambulisho wa mlipa kodi na (4) Hati ya Usuluhishi wa Mlipa Kodi (*Tax Clearance Certificate*).
4. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika eneo ambapo magogo yapo kwa tarehe iliyoonyeshwa katika Jedwali na utaendeshwa kwa kufuata Sheria ya Misituni Sura 323 Namba 14 ya mwaka 2002.
5. Wakala wa Huduma za Misituni Tanzania utatoa hati ya ushindi kwa mnunuzi aliyetaja kiwango cha juu kwa magogo ya kila kituo wakati wa mnada.

6. Ifahamike kuwa mnunuzi atakayefanikiwa kununua magogo hayo (Mkurungu) hataruhusiwa kusafinisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) ya mwaka 2004. Akitha, kusafirisha mazao ya Misitu nje ya nchi itaruhusiwa baada ya kuyachakata kwa Mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 69 la mwaka 2006.
7. Makampuni na watu binafsi wenye nia ya kununua magogo haya wanakaribishwa kutembelea maeneo yenye magogo hayo wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) atasiri isipokuwa siku za sikukuu kuanzia tarehe ya tangazo hili mpaka tarehe ya kufanyika mnada. Meneja wa Kanda au wasaidizi wake, pia mameneja wa Misitu wa Wilaya husika watakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi.
8. Bei ya kianzio kwa magogo ya kila kituo ni **TZS. 400,000.00 kwa meta ya ujazo (m³)** ambayo inajumuisha 'VAT' na 'CESS'.
9. Mnunuzi atakayeshinda mnada atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi katika muda wa siku tatu (3) baada ya mnada kufanyika. Fedha hii (25%) hazitarudishwa ondapo mnunuzi atashindwa kulipa 75% ya fedha itakayobaki. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku saba (07) baada ya mnada. Taratibu na maelekezo mongino juu ya ulipaji wa malipo haya yatatolowa na Meneja wa TFS Wilaya siku hiyo ya mnada na hatimaye malipo kufanyika kupitia Mfumo wa Malipo ya Serikali.
10. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay – in – slip) ya benki kwa Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) au kupitia kwa Meneja wa TFS wa Wilaya husika kama uthibitisho wa malipo si zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.
11. Mnunuzi atakayeshinda mnada atatakiwa kuondoa magogo yake katika eneo la mnada ndani ya siku saba (07) baada ya kumaliza malipo yote. Kwa kushindwa kufanya hivyo, mnunuzi atalipa **TZS 100,000.00 kwa kila siku ya ziada kama fidia ya ulinzi na gharama za kuhifadhi magogo hayo.**
12. Wateja wote wanaotarajia kushiriki katika mnada huu, watatakiwa kuwasilisha kwa maandishi nia yao ya kushiriki pamoja na nakala ya yaliyotajwa katika **Kifungu cha 3 cha Tangazo** kwa Mameneja wa TFS wa wilaya magogo husika yalipo siku tatu (03) kabla ya taroho ya kufanyika kwa mnada. Kwa yeyote atakayocholewa kuwasilisha kwa maandishi nia yake ya kushiriki katika mnada huu kwa muda uliopangwa hataruhusiwa kushiriki katika mnada.

limetolewa na

**MTENDAJI MKUU
WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA
S. L. P 40832
DAR ES SALAAM.**